

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي
مشروع تَعْلَمُ الإسلام – أصول العقيدة - سواحيلي

Samo la 4

الدرس الرابع

وفي قوله تعالى: ﴿ وَقَالَتِ الْيَهُودُ يَدُ اللَّهِ مَغْلُولَةٌ غُلَّتْ أَيْدِيهِمْ وَلُعِنُوا بِمَا قَالُوا بَلْ يَدَاهُ مَبْسُوطَتَانِ يُنفِقُ كَيْفَ يَشَاءُ ﴾ [المائدة: 64]

Miongoni mwa sifa za Allah (sw) anasema: ("Na mayahudi walisema, mkono wa mwenyezi mungu umefungwa kutotenda mema, mikono yao ndiyo iliyofungwa, na mwenyezi mungu amewafukuza kutoka kwenye rehema yake kwa sababu ya neno lao, bali mikono yake miwili imekunjuliwa, anatoa namna atakavyo") (Al- maidah: 63).

Anathibitisha Allah (sw) kwenye ayah hii kuwa anayo mikono miwili iliyosifika kwa ukunjufu wa kutoa zaidi kuwapa waja wake, kwa hiyo ni wajibu kuamini hivyo kuwa Allah (sw) anayo mikono miwili yenye kutoa iliyojaa neema mbali mbali, lakini ni lazima kuamini hivyo bila ya kujengea picha kwenye akili zetu, wala ndimi zetu kwa kutamka namna ilivyo hiyo mikono miwili ya Allah (sw) na kuifananisha na mikono ya viumbe vyake.

قال تعالى: ﴿ لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ﴾ [الشورى: 11]

Allah (sw) anasema: ("Mwenyezi Mungu hana mfano wake na chochote, na yeye ni mwenye kusikia na kuona ") (Al-shurah: 11).

Ufupi wa maneno katika aina hii ya Tauheed, ni kwamba ni wajibu juu yetu kuyathibitisha yote aliyoyathibitisha Allah (sw) yeye mwenyewe, au yale aliyothabitisha Mtume wake Muhammad (saw), na kuyakataa yale ambayo Allah mwenyewe ameyakaa au kukataliwa na Mtume wake Muhammad (saw) kutokana na majina yake Allah na sifa zake, bila ya kubadilisha, wala kufananisha au kupinga sifa miongoni mwa sifa zake Allah (sw) na kulinganisha.